# HEALTHCARE CHRISTIAN FELLOWSHIP (HCF) TANZANIA

"USHIRIKA WA KIKRISTO KATIKA HUDUMA ZA AFYA TANZANIA" **(Usajili No. S.A. 14631)**

Makao Makuu: Ndani ya Jengo la Umoja wa Kujisomea Biblia, Kalenga Str., Plot No. 591, DSM, Karibu na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**C/0 Dk. E.G. Mumghamba, P.O.Box 65014, Muhimbili, Dar-es-Salaam, Tanzania**

**Simu: 0716-176478, 0768-688289; 0788-422245,**

**Au Mratibu: Ms. Maria Singano-Jalas (0769112540, 0689377861) - mratibuhcftanzania@gmail.com**

**E-Mail: hcftanzania@gmail.com, emumghamba@gmail.com, Tovuti: http://www.hcftanzania.info/**


## MUHTASARI: HCF TANZANIA

**Utangulizi:** "Healthcare Christian Fellowship (HCF) Tanzania" yaani Ushirika wa Kikristo katika Huduma za Afya Tanzania ni chama kinayoshirikisha madhehebu mbali mbali ya Kikristo hapa Tanzania kutoa huduma ya habari njema za Injili ya Yesu Kristo. HCF kimataifa ilianzishwa na Uncle Francis Grim mnamo 1936, Afrika ya Kusini, ambapo makao yake makuu yapo hadi hivi leo. Uncle Francis Grim aliitwa na BWANA mwaka 2005. Kimataifa, Afrika ya Mashariki (ambapo nchi yetu ya Tanzania ipo) inahesabiwa kama kanda ya Tisa (9) duniani ("Region 9"). Nchi husika katika Kanda hii ni pamoja na Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Ethiopia, Eritrea, Somali, Somaliland, Djbouti na Sudani ya Kusini.

**Historia fupi:** Mwanzilishi wa HCF kimataifa (Uncle Francis Grim) aliitembelea hospitali ya Muhimbili mwaka 1962 ili kutushirikisha maono ya HCF. Maono ya "HCF" yalikua kwa taratibu au kwa kasi ndogo sana ndani ya mioyo ya watanzania wachache. Mnamo mwaka 1987, HCF Tanzania ilianza shughuli zake rasmi kama idara maalum chini ya Uongozi wa Umoja wa Kujisomea Biblia (UKB) Tanzania. Makao makuu ya HCF Tanzania yapo katika jengo la UKB, mtaa wa Kalenga, No. 591, Upanga-Dar, karibu na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**Usajili wa HCF Tanzania:** Septemba 23, 2013 tulipata usajili Serikalini (No. SA 14631) chini ya Sheria ya Vyama nchini Tanzania (Cap 337 R.E. 2002). Tunamshukuru sana Mungu kwa Usajili huu.

**Madhumuni:** Kuhamasisha wafanyakazi Wakristo walio katika sekta ya afya kutoa huduma kamili ya kiroho kwa jina la Yesu Kristo kwa moyo wa upendo na huruma kwa yeyote yule atakayependa kwa hiari yake mwenyewe kupokea huduma hii, hasa wagonjwa, jamaa zao na watumishi wote walio katika huduma za afya. Je unajua ukweli huu kuwa duniani kote, "***Watu wengi zaidi hupita katika vituo mbali mbali vya huduma za afya kuliko makanisani".*** Watu wote hawa wanahitaji habari njema kwamba, Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee, Yesu Kristo ili kila mtu amwaminiye asipotee katika moto wa milele bali awe na uzima wa milele. Kwa sababu hiyo, Yesu Kisto ni Bwana na Mwokozi wa ulimwengu. Watumishi Wakristo walio katika sekta ya afya wanapojitoa kuwasaidia kiroho watu wanaopita mikononi mwao wapate kuyakabidhi maisha yao kwa Bwana Yesu, wanapata wokovu, afya na matumaini tele katika ulimwengu wa sasa na ule ujao wa milele na hivyo wanapona hukumu ya kwenda kwenye moto wa milele. ***Kwa msingi huu, huduma ya HCF ni mkono wa makanisa hai ya Kikristo ndani ya hospitali na mahali popote wanapotoa huduma za afya hapa Tanzania na ulimwenguni pote.*** Kwa sababu hii tunashirikiana na makanisa ya madhehebu mbali mbali ya Kikristo yanayoamini kuwa Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi wa ulimwengu na kwamba alikuja katika mwili, akahudumu katika nguvu za Roho Mtakatifu, akafa msalabani, akazikwa, na siku ya tatu akafufuka, na alipaa mbinguni, yu hai tena milele na milele, na kwamba atarudi tena hapa duniani kulichukua "Kanisa" lake mbinguni.

**Shughuli za HCF Tanzania:** Shughuli za HCF Tanzania zimegawanyika katika sehemu tatu: Uinjilisti, Maombi na Mafundisho ambapo Yesu Kristo ndio msingi wa huduma hii. Katika matawi yote ya HCF na wakati wa makongamano ya Kitaifa kunakuwa na nafasi maalum kwa ajili ya kujifunza Neno, kufanya maombi na maombezi, kutembelea wagonjwa waliolazwa hospitalini na kuwahudumia kwa Neno la Mungu.

**Huduma za "HCF Tanzania" zimesambaa** katika hospitali zenye wanachama hai nazo ni **DSM:** Muhimbili (MNH, MUHAS, MOI, JKCI), Ocean Rd. Cancer Institute, Kairuki Hospital, Aga Khan, Mwananyamala, Amana, Tumaini-Upanga, Mt.Ukombozi-Morrocco, St. Monica-Manzese, St. Glory-Kimara, Hindu Mandal, Regency, Mbezi Health Centre-Kimara, na Magomeni Mikumi dispensary binafsi, CCBRT na Temeke Hospital. **Kilimanjaro:** KCMC, Mawenzi, Kibongoto, Moshi DC, Hai, Same, na Gonja. **Dodoma:** Mvumi Mission, Mirembe, Dodoma-Goverment Hospital, na Makole health Centre, St. John's University of Tanzania. **Njombe:** Ilembula, Kibena hospital. **Iringa:** Iringa; **Morogoro:** Morogoro, Uzima-TAG-Morogoro, na Lugala Lutheran

Hospital. **Tanga:** Bombo-Tanga, Korogwe - Magunga hospital, St. Joseph Health Centre-Kwamndolwa, Bungu Health Centre, Handeni hospital, Lushoto, Muheza DDH, Kassa; **Manyara:** Karatu na **Songwe:** Mbozi. **Arusha:** Mt. Meru, AICC, na Seliani (ALMC); **Mbeya:** Mbeya Rufaa, Meta, na Tukuyu. **Mtwara:** Newala; **Mwanza:** Bugando, Sekouture, Nyamagana; Buzuruga, Tandabuye, Makongoro-KKKT na AICT. **Mara:** Shirati, Rao, Nyerere DD. **Singida:** Singida, Sokoine, Kiomboi. **Pwani:** Kibaha na Bagamoyo. **Manyara:** Manyara. **Tabora:** Kitete. **Kigoma:** Maweni, **Shinyanga:** Kahama; **Zanzibar:** Mnazi Mmoja.

**Matawi yaliyo njiani kuthibitishwa**: **Dar:** Sinza, Mbagala Rangi Tatu, Dar-Group, UDSM-Health Centre, IMTU, St. Bernard, Masana na Rabininsia; **Kagera:** Bukoba, **Kilimanjaro:** Machame; **Mtwara:** Mtwara; **Lindi:** Lindi, n.k. ***Je, unajua hospitali au kituo ambacho bado hakijafikiwa na huduma hii? Tunakuomba utusaidie kupata mawasiliano ya uhakika na Wapendwa wa huko ili tuwasiliane nao.*** HCF Tanzania inashirikiana na wapendwa wengine ndani na nje ya nchi kwa njia ya maombi na makongamano.

**Makongamano ya Kitaifa:** HCF Tanzania imekwisha kufanya makongamano 16 hapa nchini. Mahali pa Kongamano na waandaaji ni: **Dar-es-Salaam:** National Action Team - Salvation Army (1992, 1993, 1996, 2002), Mbagala Spiritual Centre (2005 na 2012); **Kilimanjaro**: KCMC-Moshi (1997 na 2014), **Dodoma:** Mvumi Mission (1999 na 2009), Dodoma-Govt. & Mirembe Hospitals - St. John's University, Tanzania (2015); **Njombe:** Ilembula Mission Hospital (2007, *Kipindi hicho ilikuwa bado ni sehemu ya mkoa wa Iringa*); **Tanga:** Bombo Hospital (2008); **Mbeya:** Rufaa-Mbeya (2010); **Morogoro Hospitali ya Mkoa:** Bigwa-Seminary (2013); **Mwanza:** Bugando Hospital (2016); **Iringa Hospitali ya Mkoa:** Ruaha Catholic University (RUCU) 2017; **Singida Hospitali ya Mkoa: Mwenge Sekondari (**2018); Korogwe-Tanga : **St. Rock College, Korogwe** (2019) lilifanyika kwa mafanikio makubwa na lilifunguliwa na Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Kissa Kasongwa. Mahudhurio - Wajumbe 92 kutoka matawi 24 ya HCF katika mikoa 15 Tanzania. *Ushuhudiaji hospitalini na shuleni:* Roho Mtakatifu aliwagusa watu kumpokea Bwana Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yao. Tuendelee kuomba wote waendelee kumpenda Yesu Kristo na kuukulia wokovu.

## Kongamano la HCF Tanzania la 2020: Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi, Tabora (Oktoba 16-18, 2020)

***NENO KUU (Theme)*: "Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu (Rum.12:1).** Kamati ya Maandalizi (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Tabora ikishirikiana na "National Action Team (NAT) imekamilisha maandalizi yote (kipeperushi kimeambatanishwa). Tafadhalini sana tuendelee kuombea Kongamano hili wakati wote hasa kuombea afya njema za wajumbe, upatikanaji wa ruhusa, fedha na ulinzi safarini. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii (Yak. 5:16b).

**Makongamano ya Kimataifa:** Siku zilizopita, wana-HCF Tanzania walihudhuria makongamano mbali mbali nje ya nchi ikiwemo S.Afrika, Uingereza- Exeta, Uganda, Kenya, na Manila-Phillipines (2011 = Diamond Jubilee - miaka 75 ya HCFI (Wawakilishi: Ms. M. Philemon na Ms.G. Sabuka); maombi ya ulimwengu mzima (Global Prayer Summit (GPS)) Wales-Uingereza 2015 (Mwakilishi: Dk.E. Mumghamba). Mwaka 2017 GPS ilifanyika Sri Lanka Mwakilishi: Mratibu wa HCF Region 9, Mr. B. Bakunda- Uganda). Kongamano la Afrika Mashariki, Region-9, Kigali, Rwanda (Mei 17-21, 2018) Wawakilishi: wajumbe 11 (Dar-7, Mbeya-1 na Tanga-3). **Maombi ya HCF Ulimwengu mzima (Global Prayer Summit (GPS) – 2019**, Oktoba 13-18: Pretoria, S.Africa *Semina ya Viongozi wa HCF: eMseni Conf. Centre (Oktoba 18-22, 2019)* ambapo tuliwakilishwa na wajumbe saba (Ms. M.Philemon (DSM), Dk.Sr. A. Temba & Dk. A.Mpemba (Korogwe), Dk. G. Samba & Sr. H. Salim (Bombo, Tanga), Sr. N.Kileo (Muhimbili-DSM). Kongamano la Uganda Reg.9 halikufanyika kutokana na tatizo la tauni ya Covid-19. Linategemewa kufanyika mwakani (2021) tuendelee kuomba.

**Mapato: Mapato ya HCF Tanzania hutokana na sadaka (60% kutoka matawini) na michango ya 1/30 mshahara kila mwezi kutoka kwa wana-HCF waaminifu.** Tafadhali, michango yote ya fedha itumwe moja kwa moja kwa Mtunza Hazina wa HCF-Tanzania Mr. Godwin Magwira (M-Pesa: 0764-753093, Tigo-Pesa: 0654-385713, Airtel-Money: 0789-103391 AU ipelekwe Benki NMB Akaunti Na: 2096600029, Healthcare Christian Fellowship (HCF), Tanzania, AU NBC, Akaunti Na: 041201043597, Scripture Union, Dept. of Hospital Christian Fellowship. **Mungu azikumbuke sadaka zako zote... Akujalie kwa kadiri ya haja ya moyo wako (Zab.20:3-4) na BWANA akubarikie na kukulinda utokapo na uingiapo (Kumb.Tor.28:6, Zab.121:8).**

**Uongozi:** Mwenyekiti, Makamu M/kiti, Katibu, Mtunza Hazina, na Wajumbe wa NAT kutoka Kanda mbali mbali za HCF Tanzania (mikoani na makao makuu-DSM) wapo na huchaguliwa na wanachama katika mkutano mkuu wa mwaka kila baada ya miaka mitatu. Pia ipo nafasi ya Mratibu, mwajiriwa pekee tangu 2014 na hulipwa mshahara kila mwezi kutokana na makusanyo ya 60% ya sadaka na michango yetu ya 1/30 ya mishahara yetu ya kila mwezi kama makao makuu ya HCF ulimwenguni (HCFI) yalivyoelekeza) kwa shughuli za HCF-Makao Makuu na Tanzania nzima.

Dk. Elifuraha G. Mumghamba (DDS, Mdent, PhD) Oktoba 6, 2020
**M/KITI: HCF TANZANIA**

E.2020/ HCF-2020/ MUHTASARI-v144a HCF-TZ Sgned (6.10.2020 T23.35pm) HCF in Short ni Nini